**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

## TATHMINI YA SAFARI ZA MABASI KWA RATIBA ZA USIKU KWA KIPINDI CHA KUANZIA TAREHE 01 OKTOBA - 06 NOVEMBA 2023

**Ndugu Wanahabari,** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ina dhamira ya kweli ya kuimarisha shughuli za uchumi wa Wananchi wake wote wa maeneo ya mijini na vijijini kwa kuboresha miundombinu ya usafiri pamoja na vyombo vya usafiri wa umma kwa lengo la kuchochea shughuli za kiuchumi, kijamii na kuongeza mchango wa Sekta Binafsi kwenye kuchangia pato la Taifa.

Mtakumbuka kwamba, mnamo tarehe 28 Juni, 2023, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakatia akiahirisha Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jijini Dodoma, alitoa tamko la maamuzi ya Serikali kuondoa zuio la mabasi kusafiri kwa saa 24. Hatua hii ya Serikali ilizingatia maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo Wabunge, wamiliki wa mabasi, madereva wa mabasi, wasafiri, wafanya biashara na wananchi kwa ujumla. Aidha, Waziri Mkuu alielekeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ishirikiane na Wizara ya Uchukuzi kuweka utaratibu wa safari hizo.

**Ndugu Wanahabari,** Mtakumbuka kwamba, Mhe. Jumanne Sagini, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, tarehe 29 Septemba, 2023, alitoa taarifa ya kuanza kwa safari za mabasi kwa saa 24, kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2023. Taarifa hii ya Mhe. Sagini, ilitolewa baada ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Uchukuzi kukamilisha maandalizi na taratibu za kuzingatiwa kwa wasafirishaji watakaotaka kutoa huduma za safari za usiku (saa 24). Hivyo, wasimamizi wa utekelezaji wa maamuzi haya ya Serikali ni LATRA na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani.

**Ndugu Wanahabari,** Kabla ya Serikali kutangaza kuanza kwa ratiba za usiku tarehe 1 Oktoba, 2023, LATRA ilikutana na watoa huduma (wamiliki wa mabasi) wakiongozwa na Chama cha Wamiliki wa -TABOA, tarehe 7 Septemba, 2023 na kukumbushana kuzingatiwa kwa Sheria, Kanuni na Taratibu zitakazotolewa wakati wa kuanza kwa safari za saa 24. LATRA ilipokea maoni ya wadau hawa muhimu (TABOA na wasio wanachama wa TABOA) katika kukamilisha taratibu zilizotangazwa na Mhe. Sagini, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani.

Miongoni mwa mambo muhimu tuliyokumbushana ambayo pia yameelekezwa kwenye Sheria ya Mamalaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sheria za Usalama Barabarani pamoja na Kanuni za Huduma za Usafiri wa Umma ni pamoja na kuhakikisha;

(i) mabasi yameuganishwa kwenye mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS);
(ii) madereva wamesajiliwa kwenye mfumo wa utambuzi na kutumia kitufe cha utambuzi (i button);
(iii) kuwa na madereva wawili kwa mabasi yafanyayo safari za masafa marefu zaidi ya kilomita 700;
(iv) kutumia Tiketi Mtandao na Orodha ya Abiria Wanao Safiri (Manifesti) iwe inatolewa kwa njia ya Kielektroniki;
(v) kuzingatia ukomo wa mwendokasi (speed) kwa mujibu wa Sheria na Kanuni na;
(vi) Mizigo ya abiria kuwekwa tagi za utambulisho

.

**Ndugu Wanahabari,** Hadi kufikia tarehe 06 Novemba, 2023 Mamlaka imetoa ratiba za usiku kwa mabasi 246 kwa kampuni/ wasafirishaji 46 na kwa jumla ya njia 26 zinazoanzia jijini Dar es Salaam. Tafsiri hii inaonesha kunamwitikio mkubwa wa safari za usiku. Kwa ujumla, usafiri wa mabasi kwa saa 24 unaungwa mkono na watumia huduma walio wengi na inaboresha shughuli za kijamii na kiuchumi.

Hata hivyo, katika kufuatilia mwenendo wa utoaji huduma kwa kutumia nyenzo mbalimbali zikiwemo, Mfumo wa VTS, ratiba za mabasi, ukaguzi wa maeneo mbalimbali, yafuatayo yamebainika:

(i) mabasi yameuganishwa kwenye VTS lakini baadhi zimekuwa hazitumi taarifa kabisa, zikituma taarifa kwa kurukaruka na kuchezewa kwa mfumo (VTS);

(ii) madereva kubainika kutotumia i-button, pengine hawajasajiliwa, wanasafiri dereva mmoja kwa basi, au wanaenda safari ya usiku na kurudi mchana bila kupumzika vya kutosha;

(iii) kuwepo vituo vya ukaguzi wa safari ndefu na ubadilishanaji wa madereva lakini kukosekana kwa taarifa ya ubadilishanaji ambao tungeuona pia kwa i-button;

(iv) kutumia Tiketi Mtandao bila kutoa Orodha ya Abiria Wanao Safiri (Manifesti) na kuwapatia Jeshi la Polisi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo;

(v) mabasi mengi yamebainika kusafiri kwa mwendo kasi wakati wa usiku kuliko mchana, jambo ambalo ni hatari kwa abiria, chombo cha usafiri na watumiaji wengine wa barabara; na;

(vi) wahudumu wa mabasi mengi hawaweki tagi za utambulisho kwenye mizigo ya abiria hususan zinazowekwa kwenye buti. Hivyo, tumekuwa tukipokea malalamiko kila wiki ya kupotelewa mzigo.

**Ndugu Wanahabari,** Tathmini yetu imebaini kwamba zaidi ya 98% ya mabasi yote yanatumia mfumo wa Tiketi Mtandao, lakini, taarifa za abiria haziingizwi ipasavyo ikiwemo kutoacha orodha ya abiria (manifest) kwenye vituo vya kuanzia safari.

Kati ya mabasi 246 mabasi 197 sawa na 80% ya mabasi yanaendwa mwendo kasi kati ya kilometa 86-89 kwa saa na 09% wanaendesha mwendokasi kati ya kilometa 90 – 103 kwa saa, ambapo LATRA na Jeshi la Polisi tumechukua hatua zifuatazo:

(i) mabasi yaliyokamatwa kwa mwendo kasi na kuchezea mfumo wa VTS ni 759;

(ii) Mabasi yaliyopewa onyo ni 723;

(iii) mabasi yaliyositishiwa leseni zao mapaka Mamlaka itakapo jiridhisha kuwa wamebadilika ni 36. Kampuni zilizoongoza katika kuchezea mfumo wa VTS na mwendokasi ni kampuni ya Kapricon ambapo jumla ya mabasi 09 yalifungiwa, Abood Bus (mabasi 02), Dar Express (mabasi 02) na kampuni 23 zilifungiwa basi moja moja.

(iv) madereva waliofungiwa kwa kuchezea mfumo ni 10;

(v) madereva walioandikiwa faini kwa makosa ya mwendokasi ni 666;

(vi) madereva waliofikishwa mahakamani ni 32; na

(vii) madereva walio onywa ni 50.

**Ndugu Wanahabari,** Orodha ya mabasi yaliyositishiwa leseni na madereva waliofungiwa imeambatishwa na taarifa hii (Angalia Kiambatisho A na B). Wananchi na watoa huduma wanakumbushwa kutimiza wajibu wao na kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu ili kuendana na azma ya Serikali ya kuruhusu utoaji huduma kwa saa 24. Uzingatiaji huo wa sheria, ni kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Sura ya 413, na Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 na Kanuni zake.

Madereva hawa hawaruhusiwi kuendesha gari lolote kwa kipindi chote cha kutumikia adhabu. Baada ya kutumikia adhabu, ili kurejeshewa madaraja ya leseni zao, dereva atalazimika kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 kifungu cha 23 na kifungu cha 28(6).

**Ndugu Wanahabari,** Baada ya kumaliza kutumikia adhabu, Dereva atatakiwa kuomba kufunguliwa na Ofisi ya Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani ambapo kabla ya kufunguliwa atalazimika kutahiniwa ili kupimwa uwezo wake kwenye taaluma ya udereva. Na iwapo atafaulu atarejeshewa madaraja ya leseni yake kama atatetea sifa ya kuendelea kumiliki madaraja hayo.

**Asanteni Sana**

*Imetolewa na :*

| | |
|---|---|
| ............................................ | ............................................ |
| CPA Habibu J. Suluo | SACP Ramadhani Ng'anzi |
| **MKURUGENZI MKUU** | **KAMANDA WA POLISI** |
| **MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI** | **KIKOSI CHA USALAMA BARABARANI** |

**09 NOVEMBA, 2023**

**Kiambatisho A: Orodha ya Mabasi Yaliyositishiwa Leseni**

| NA. | TAREHE YA KUFUNGIA | NAMBA YA USAJILI | JINA/KAMPUNI | NJIA | SABABU YA KUSITISHA LESENI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 18/10/2023 | T819 DXJ | Abood Bus Service | Dar es Salaam -Bukoba | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 2 | 19/10/2023 | T901 DKY | Abood Bus Service | Dar es Salaam -Tabora | Kuchezea mfumo |
| 3 | 18/10/2023 | T872 DPA | Aiman Munir Abdalah | Dar es Salaam - Nanjilinji | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 4 | 17/10/2023 | T562 CAP | Antonia Zakaria | Mwanza - Musoma | Kutotuma taarifa |
| 5 | 18/10/2023 | T445 DCW | Basil Blasto Makundi | Dar es Salaam - Turiani | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 6 | 16/10/2023 | T126 DKW | Batco Safari | Mwanza - Ngerengere | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 7 | 02/10/2023 | T154 CYZ | Burudani Express | Dar es Salaam- Lushoto | Kuchezea mfumo |
| 8 | 02/10/2023 | T652 DPM | Dar Express | Dar es Salaam - Tarakea | Kutotuma taarifa |
| 9 | 04/10/2023 | T899 EDQ | Dar Express | Dar es Salaam- Karatu | Kuchezea mfumo |
| 10 | 30/10/2023 | T193 DZU | Frester Investment | Dar es Salaam- Bukoba | Kuchezea mfumo |
| 11 | 16/10/2023 | T798 DPP | Hajee Safaris LTD | Dar es Salaam - Handeni | Kutotuma taarifa |
| 12 | 09/10/2023 | T204 DQB | JM Couriers LTD | Dar es Salaam- Kiomboi | Kuchezea mfumo |
| 13 | 19/10/2023 | T728 EBJ | Johanvia Investment | Dar es Salaam - Musoma | Kuchezea mfumo |
| 14 | 20/10/2023 | T473 CJN | Joseph M Mwita | Tabora - Mbeya | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 15 | 02/10/2023 | T131 DRE | Kapricon | Dar es salaam- Musoma | Kuchezea mfumo |
| 16 | 05/10/2023 | T607 DJR | Kapricon | Dar es Salaam- Musoma | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 17 | 05/10/2023 | T835 DUJ | Kapricon | Dar es Salaam- Musoma | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 18 | 05/10/2023 | T564 DRE | Kapricon | Dar es Salaam- Arusha | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 19 | 05/10/2023 | T605 DJR | Kapricon | Dar es Salaam- Mwanza | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 20 | 05/10/2023 | T612 DJR | Kapricon | Dar es Salaam- Mwanza | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 21 | 17/10/2023 | T258 DHM | Kapricon | Arusha- Kigoma | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 22 | 17/10/2023 | T290 DAJ | Kapricon | Dar es Salaam - Arusha | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |

| NA. | TAREHE YA KUFUNGIA | NAMBA YA USAJILI | JINA/KAMPUNI | NJIA | SABABU YA KUSITISHA LESENI |
|---|---|---|---|---|---|
| 23 | 17/10/2023 | T688 DPS | Kapricon | Shinyanga  Tanga | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 24 | 19/10/2023 | T186 DGD | Kimotco Intertrade Company LTD | Arusha - Njombe | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 25 | 10/10/2023 | T110 DLV | Masalu High Class | Mwanza- Moshi | Kuchezea mfumo |
| 26 | 17/10/2023 | T674 DEN | Nassoro Athumani Sungata | Itigi - Mwanza | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 27 | 19/10/2023 | T853 DUW | Simba Mtoto | Dar es Salaam - Tanga | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 28 | 19/10/2023 | T345 DXJ | Super Feo | Tunduru - Mbeya | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 29 | 02/10/2023 | T230 BRJ | Takbir Logistics Company LTD | Mwanza- Kigoma | Kuchezea mfumo |
| 30 | 09/10/2023 | T994 DQT | Tashriff Trans | Dar es Salaam - Tanga | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 31 | 02/10/2023 | T377 CAX | Tokyo Takara | Dar es Salaam- Masasi | Kuchezea mfumo |
| 32 | 30/10/2023 | T275 DXW | Travel Partner Limited | Dar es Salaam - Bukoba | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 33 | 02/10/2023 | T98O DPZ | Tungi Express | Mwanza - Mutukula | Kutuma taarifa kwa kurukaruka |
| 34 | 30/10/2023 | T362 EED | Ubaruku Constraction Company | Dar es Salaam -Ubaruku | Kuchezea mfumo |
| 35 | 02/10/2023 | T956 DDH | Yehova Yire | Bukoba -Kigoma | Kutotuma taarifa |
| 36 | 20/10/2023 | T361 ALU | Zube Trans | Mwanza- Ngara | Kutotuma taarifa |

**Kiambatisho B; Orodha ya Madereva Waliofungiwa Leseni**

| NA | PICHA YA DEREVA | TAARIFA ZA DEREVA NA SABABU YA KUFUNGIWA |
|---|---|---|
| 01 |  | **JINA:** AHMED SALUM SALAMA<br>**NA. YA LESENI:** 4001424109<br>**KAMPUNI:** JOHANVIA INVESTMENT LTD<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 24 Oktoba, 2023 hadi 23 Novemba, 2023 kwa kosa la kuchezea kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD) na kusababisha mfumo wa VTS wa gari Na. **T728 EBT** kushindwa kufanya kazi wakati wote wa safari. |
| 02 |  | **JINA:** JUMAA SEIF NASSORO<br>**NA. YA LESENI:** 4000190738<br>**KAMPUNI:** KIMBINYIKO<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 09 Oktoba, 2023 hadi 08 Novemba, 2023 kwa kosa la kuendesha basi kwa mwendo hatarishi.<br><br>Kati ya Septemba 19-20, 2023 aliendesha basi Na. **T462 DQG** kwa mwendokasi hadi kilomita 91 kwa saa. |

<table>
<tr>
<td>03</td>
<td></td>
<td>JINA: JUMA RAMADHANI MBEGA<br>NA. YA LESENI: 4002956665<br>KAMPUNI: MONGE M. KAHONGE<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha miezi miwili kuanzia tarehe 10 Oktoba, 2023 hadi 09 Desemba, 2023 kwa kosa la kuchezea kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD) na kusasabisha mfumo wa VTS wa gari Na. T148 DYR kushindwa kufanya kazi wakati wote wa safari.</td>
</tr>
<tr>
<td>04</td>
<td></td>
<td>JINA: PAULO SAMSON WAMBURA<br>NA. YA LESENI: 4000242471<br>KAMPUNI: MACHAME EXPRESS<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 09 Oktoba, 2023 hadi 08 Novemba, 2023 kwa kosa la kuendesha basi kwa mwendo hatarishi.<br><br>Kati ya Septemba 19-20, 2023 aliendesha basi Na. T772 EDY kwa mwendo hatarishi hadi kilomita 100 kwa saa.</td>
</tr>
<tr>
<td>05</td>
<td></td>
<td>JINA: IZACK VIANI VELATA<br>NA. YA LESENI: 4000386035<br>KAMPUNI: HAPPY NATION EXPRESS<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 09 Oktoba, 2023 hadi 08 Novemba, 2023 kwa kosa la kuendesha basi kwa mwendo hatarishi.<br><br>Kati ya Septemba 19-20, 2023 aliendesha basi Na. T523 DUH kwa mwendokasi hadi kilomita 90 kwa saa.</td>
</tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| **06** |  | **JINA:** PATRICK MAMFERE SHOO<br>**NA. YA LESENI:** 4005231398<br>**KAMPUNI:** IMANI PETER SHOO<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 05 Oktoba, 2023 hadi 06 Novemba, 2023 kwa kosa la kusababisha ajali ya pikipiki na kusababisha madhara kwa dereva wa pikipiki na abiria wake. |
| **07** |  | **JINA:** JUMA SALUM KIKWEMBE<br>**NA. YA LESENI:** 4000141727<br>**KAMPUNI:** SAIBABA EXPRESS<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2023 hadi 28 April, 2024 kwa kosa la kuendesha basi kwa mwendo hatarishi.<br><br>Mnamo Oktoba 24, 2023 aliendesha basi Na. **T973 AVW** kwa mwendo hatarishi hadi kilomita 112 kwa saa. |
| **08** |  | **JINA:** ISMAIL YAHYA MARIJANI<br>**NA. YA LESENI:** 4001058860<br>**KAMPUNI:** KWAYA KUU RUANDA MORAVIAN<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2023 hadi 28 April, 2024 kwa kosa la kuendesha basi kwa mwendo hatarishi.<br><br>Kati ya Septemba 19-20, 2023 aliendesha basi Na. **T725 ECC** kwa mwendokasi hadi kilomita 113 kwa saa. |

| | | |
|---|---|---|
| **09** |  | **JINA:** EMANUELY ERIUD MSYANI<br>**NA. YA LESENI:** 4001722237<br>**KAMPUNI:** BAHARI GROUP<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2023 hadi 28 April, 2024 kwa kosa la kuendesha basi kwa mwendo hatarishi.<br><br>Mnamo Septemba 5, 2023 aliendesha basi Na. **T855 DYG** kwa mwendokasi hadi kilomita 121 kwa saa. |
| **10** |  | **JINA:** MICHAEL MAXIMILIAN KITENGULE<br>**NA. YA LESENI:** 4000379563<br>**KAMPUNI:** FRESTER INVESTMENT LTD<br><br>Amefungiwa leseni ya udereva kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia tarehe 10 Oktoba, 2023 hadi 11 Novemba, 2023 kwa kosa la kuendesha basi kwa mwendo hatarishi.<br><br>Kati ya Septemba 19-20, 2023 aliendesha basi Na. **T348 DUH** kwa mwendo hatarishi hadi kilomita 100 kwa saa. |